**BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU**

**KIDATO VI**

**KISWAHILI 2**

**121/2** **(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)**

**MUDA: Saa 3:00** **Jumatano, 4 Machi 2026 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali nane (8).
2. Jibu maswali **yote** kutoka sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali **la tano (5)** ni la lazima.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Shulelibrary.com

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Soma shairi lifuatalo kisha eleza mbinu za kifani zilizojitokeza katika kazi hiyo.

Kuna hadithi ya kale, kwa babu nimepokea
Kwa manyani zama zile, mkasa ulotokea
Nilikuwa mwanakele, hayo nikazingatiya
Leo nawadokezeya, kwa nilivyoyafahamu.

Nyani bada kugundua, watu wanawaviziya
Sababu yake kwa kuwa, huila yao mimeya
Na ndipo wakaanuwa, mwenzao kumtumiya
Ende akawalimye, mazao yalo muhimu.

Kwenye uamuzi huo, baada ya kukusudiya
Kibwangai jama yao, wakamkata mkiya
Unyani kwa mbinu zao, kwake ukajitokeya
Akawa yeye si nyani, bali ni binaadamu.

Yalisudi watakayo, nyani wakafurahiya
Yaliposadifu hayo, wote wakachekeleya
Walidhani watakayo, atawakamilishiya
Nyoyo zikategemeya, na nyuso kutabasamu.

Bwana mmoja kasema, kibwangai kumwambiya
Kama tutakalokutuma, weza kututimiziya
Isiwe kurudi nyuma, we mwenzetu sikiya
Wewe tumekuchaguwa, utumikiye kaumu.

Kibwangai akasema, hayo nimezingatiya
Kidete nitasimama, jitihada kutumiya
Kwa kusia na kulima, mpate jifaidiya
Sitobadili mawazo, ilipwe yangu kaumu.

Shulelibrary.com

Kibwangai alipoona, ni mtu kakamiliya
Akaanza kujivuna, na dharau kuzidiya
Wala hakujali tena, wenzake walomwambiya
Akahisi hawi nyani, umbo lile litadumu.

Kawa na tabia moja, nyani walipomwendeya
Akajifunga mkaja, mijiwe kuwarushia
Hakujali zao haja, wala kuwahurumiya
Kapiga na kukeneya, pia na kuwashutumu.

Nyani likawa - kasri, ghadhabu wakaingiya
Wakafanyiza shauri, kibwangai kumwendeya
Kwa nguvu au hiari, kumpa wake mkiya
Ili awe nyani tena, asiwe binaadamu.

Mkia bada kumpa, mambo yakawa mabaya
Nguo zake kuzitupa, unyani kumrudiya
Kaanza kuchupa chupa, mtini akarukiya
Akawafata wenzake, akiwa nyani katimu.

Wenzake wakamcheka, wote na kumzoeya
Akakosa la kushika, kwa haya kujioneya
Majuto yakamfika, akabakia kuliya
Akarudi porini, iliko yake kaumu.

2. "Mwalimu Tito ni mtambaji mzuri wa kazi mbalimbali za fasihi simulizi, mwenye sifa pambanuzi ambazo huwezi kuzikuta kwa mtambaji mwingine." Ukiwa miongoni mwa wanafunzi wake hodari, thibitisha ukweli wa kauli hiyo. Toa hoja tano (5).

3. Licha ya juhudi zilizofanywa na Baraza la Sanaa na wasanii nchini Tanzania, lakini bado takwimu zinaonesha kuwa sanaa za maonesho zinazidi kufifia na kupoteza mwelekeo wake kabisa. Ukiwa kama mbobezi katika uga huu, eleza chanzo cha kutokea kwa hali hiyo. Toa hoja tano (5) na mifano.

Shulelibrary.com

4. Madenge ni msanii maarufu wa nyimbo na maigizo anayefanya kazi chini ya kampuni ya simu ya Nokia hapa nchini, baada ya kupata udhamini mnono wa miaka kumi. Kama mwanafasihi mwerevu, eleza madhara yanayoweza kujitokeza katika kazi zake. Toa hoja tano (5) na mifano.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali matatu (3) katika sehemu hii. Swali la **tano (5)** ni la lazima.

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| Kimbunga | - | Haji Gora |
| Mapenzi Bora | - | Shabani Robert |
| Chungu Tamu | - | Theobald A. Mvungi |
| Fungate ya Uhuru | - | Mohammed S. Khatibu |

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| Usiku Utakapokwisha | - | Mbunda Msokile |
| Kufikirika | - | Shabani Robert |
| Mfadhili | - | Hussein Tuwa |
| Vuta N'kuvute | - | Shafi Adam Shafi |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| Kwenye Ukingo wa Thim | - | Ebrahim Hussein |
| Morani | - | Emmanuel Mbogo |
| Kivuli Kinaishi | - | Said Mohamed |
| Nguzo Mama | - | Penina Muhando |

Shulelibrary.com

5. Mtindo ni dhana telezi, kwani namna inavyojadiliwa katika ushairi ni tofauti na namna inavyojitokeza katika kazi nyingine za fasihi. Kwa kutumia diwani mbili ulizosoma, onesha namna watunzi wa ushairi walivyoogelea na kukata mawimbi katika bahari yao. Toa hoja tatu (3) kwa kila kitabu.

6. "Wasanii wengi wa Tanzania ni werevu wa jamii watokazo." Kwa kutumia diwani mbili ulizosoma, jadili jinsi wasanii hao walivyoakisi jamii kupitia kazi zao za sanaa. Toa hoja nne (4) kwa kila diwani uliyosoma.

7. Watunzi wa tamthiliya ni wajuzi wa kuzipamba kazi zao kwa njia tofauti tofauti ili kuongeza mvuto katika kazi za fasihi. Kwa kutumia jazanda mbalimbali, thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja nne (4) kwa kila kitabu.

8. "Tamaa mbele mauti nyuma", ni kauli ya wahenga inayoendelea kutumika hadi leo katika jamii zetu. Kwa kutumia wahusika wawili kwa kila kitabu, onesha namna wahenga walivyoona mbali kwa kuibua migogoro iliyotokana na tamaa zao. Toa hoja nne (4) kwa kila kitabu cha riwaya ulichosoma.

*Wabillah Tawfiiq*

Shulelibrary.com